SURA YA KUMI NA TANO

# TATHMINI YA TAFSIRI YA PENDEKEZO LA KATIBA YA KENYA 2010

Grace Wanja na Miriam Osore

## Utangulizi

Makala hii inanuia kutathmini kielelezo patanifu cha Katiba ya Kenya, nakala ya Kiswahili. Hili ni pendekezo la katiba ya Kenya lililochapishwa Mei 6, 2010 katika lugha ya Kiswahili. Kusudi ni kuona udhaifu uliokuwepo kwenye tafsiri hiyo ya katiba; udhaifu ambao kwa maoni yetu uliifanya nakala hii ya Kiswahili kutoakisi kwa usahihi yale yaliyokuwa katika nakala ya Kiingereza.

Makala hii inazo sehemu sita. Sehemu ya kwanza ni utangulizi huu. Sehemu ya pili inahusu historia fupi ya uundaji wa katiba nchini Kenya. Hii inafuatwa na misingi ya kinadharia ambayo itaongoza uchambuzi wa makala hii. Sehemu ya nne inafafanua upekee wa sajili ya kisheria na katika sehemu ya tano kunabainishwa baadhi ya makosa yaliyojitokeza katika nakala ya tafsiri ya Kiswahili ya hiki kielelezo patanifu cha katiba ya Kenya. Sehemu ya sita ni hitimisho la makala yote.

## Historia ya uundaji Katiba Nchini Kenya

Katiba ni makubaliano ambayo yanaeleza muundo wa kimsingi na kanuni za uongozi katika shirika, ikiwa ni pamoja na haki na majukumu ya washirika wa shirika hilo. Katiba ndiyo sheria ya kimsingi ya nchi ambayo huwaelekeza viongozi yale wanayoweza kufanya. Katiba ni msingi wa kisheria wa taifa unaomilikiwa na raia wote kwa kiwango sawa kama vile taifa lenyewe linavyomilikiwa.

Neno la Kiingereza *Constitution* (Katiba) linatokana na neno la Kilatini 'constitutio'. Lilikuwa likitumiwa kumaanisha kanuni na marekebisho ya sheria kama vile sheria za kifalme. Baadaye neno hili lilitumiwa kumaanisha kanuni za sheria za kanisa zilizoitwa *canon law*. Sheria hizi

zilitumiwa kueleza mambo muhimu kama vile amri iliyotolewa na Askofu Mkuu wa kanisa la Kirumi, ambazo sasa huitwa katiba ya mitume (Melvin 2010).

Katiba basi inaweza kuchukuliwa kama sheria ambazo zinatumiwa na serikali ama kikundi fulani cha watu waliokubaliana kutawaliwa kupitia sheria hizo. Sheria hizo zinaweza kuwa zimeandikwa na hutumika kuweka mipaka ya mamlaka katika kikundi hicho. Gicheru na Miano (1987) wanasema kuwa katiba huhusu sheria zinazoonyesha aina ya serikali pamoja na haki na wajibu wake kwa wananchi, na pia wajibu wa wananchi kwa serikali hiyo. Wanaendelea kusema kuwa katiba ni maandishi ya kipekee yanayoonyesha mihimili inayoongoza sehemu za serikali fulani katika utendakazi. Wanasisitiza kuwa katiba lazima ionyeshe kinaga ubaga mambo yafuatayo:

1. Jinsi idara za serikali hufanya kazi.
2. Wajibu na mamlaka ya idara za serikali.
3. Jinsi mamlaka na uwezo wa idara za serikali hutekelezwa.

Makala haya yanachukulia kuwa katiba ni jumla ya kanuni ambazo kwazo huwezesha serikali kutawala nchi. Katiba ni sheria kuu ya nchi na inaunganisha asasi zote za nchi katika viwango vyote viwili; serikali na watu wote. Kwa hivyo hakuna mtu anayeweza kudai au kutumia mamlaka ya taifa ila kwa idhini ya katiba. Sheria yoyote ikiwemo sheria ya mila na tamaduni ambayo haiambatani na katiba ni batili.

Nchi nyingi ambazo huishi kwa amani na mapatano, huwa na sheria katika utawala wake. Katiba ni kitu cha kipekee katika nchi, na wananchi huwa na matumaini sana kwamba kupitia katiba ya nchi yao watapata maendeleo. Kama katiba ya nchi fulani haifuatwi, wananchi huhisi kana kwamba kutakuwa na michafuko nchini. Kama katiba inafuatwa, wananchi huhisi kwamba maisha yao ni mazuri na yatazidi kuwa yenye maendeleo kwani kutakuwa na amani nchini (Kibwana 1997).

Kenya husemekana kuwa nchi ya kidemokrasia na kwa hivyo wananchi wanapaswa kufurahia haki na uhuru wao. Wananchi wana uhuru wa kuongea, kutangamana na uhuru wa kutofungwa ovyo ovyo bila kufuata sheria na mengineyo. Haki hizi zote zimeandikwa katika katiba. Nchi zinazotumia katiba ni za kidemokrasia ambapo utawala huwa ni kwa uwakilishi wa watu waliochaguliwa na watu wenyewe. Nguvu za utawala huamuliwa na watu. Ni jambo la busara kama watu wanaelewa sheria

zinazowatawala. Mambo hayo yote yatawezekana kama katiba imeandikwa kwa lugha na njia iliyo wazi inayoeleweka bila matatizo. Maana ya demokrasia haiwezi kudhihirika vizuri kama kuna sehemu ya umma ambayo haishiriki vizuri kwa sababu ya kutoelewa katiba.

Kwa mujibu wa Kindiki na Ambani (2005), katiba ya kwanza ya Kenya ni ile iliyotoka Bunge la Lancaster. Katiba hii haikuwa na maono ya wananchi wa Kenya, wala zao la ushirika wa wakenya bali iliwasilishwa kwa wakenya na wakoloni. Ina mchanganyiko usiofaa wa mfumo wa bunge la Uingereza na mfumo wa Kimarekani. Katiba kama hiyo haiwezi kuwa bora, na haiwezi kupendwa na wananchi wa Kenya. Kindiki na Ambani wanaendelea kusema kuwa, katiba hii haikutia maanani haki za kibinandamu, na kwa sababu hiyo tangu 1963 wakati Kenya ilipopata uhuru, kumekuwa na misukosuko ya kisiasa.

Wakenya kutoka kote nchini na kutoka viwango vyote vya kijamii wamefahamu vizuri kutokana na tajiriba ya kila siku, kuhusiana na ufisadi katika huduma za umma, usimamizi mbaya wa uchumi, utumiaji nguvu katika siasa, ukosefu wa nidhamu katika idara ya polisi na matatizo mengi, kwamba katiba hiyo ya kwanza haikukidhi mahitaji na matamanio yao. Ilibidi katiba ya taifa imilikiwe na raia kwa kuwahusisha wananchi katika uundaji wake. Lengo kuu lilikuwa kuuwezesha umma kujitawala. Kibwana (2001) anasema kuwa katiba hiyo ilijaa mapengo, kutoafikiana na ukinzani. Ni katiba iliyolimbikizia mamlaka mtu mmoja huku wananchi wengi wakiteseka. Kutokana na mambo haya yote Kenya ilihitaji katiba mpya ili kuikomboa na kufuta sura hiyo mbaya na kuifanya itengenee. Kwa takriban miaka ishirini wananchi wa Kenya wamekuwa wakidai katiba irekebishwe.

Katiba ya Kenya imefanyiwa marekebisho mengi. Tume ya Marekebisho ya Katiba iliyoundwa mwaka wa 2001 iliendelea kufanyia katiba marekebisho na kushirikisha wawakilishi wa wananchi wote ambao waliweza kutoa maoni yao. Kundi hili liliweza kutoa katiba kielelezo cha Bomas ambayo iliendelea kufanyiwa marekebisho. Katiba iliyopendekezwa mwaka 2005 ilipigiwa kura ya maoni na kukataliwa na asili mia hamsini na saba ya wapigaji kura.

Mnamo mwaka wa 2008 kamati ya wataalamu ilichaguliwa ili kuendelea na marekebisho ya katiba ya Kenya. Kamati ya wataalamu iliweza kutoa kielelezo patanifu cha katiba ya Kenya ili Wakenya wasome, kujadiliana, na pia kutoa maoni yao. Katiba iliyopendekezwa ya mwaka

2010, ilitokana na marekebisho kadhaa ya kielelezo patanifu cha katiba ya Kenya. Pendekezo la katiba ya Kenya lilitolewa kwa wakenya ili waweze kusoma na kuelewa ndiposa waweze kupiga kura ya maamuzi mnamo tarehe 4 August 2010.

Wananchi walihimizwa kujisomea na kuelewa katiba hiyo ili wasije wakapotoshwa. Ili kuweza kusoma na kuilewa katiba na kuepukana na upotoshi, kulikuwa na haja ya nakala hii muhimu kutafsiriwa kwa lugha mbalimbali ili ieleweke kwa kila Mkenya. Nakala hii ya Kiswahili nidyo inayotathminiwa katika makala haya. Tathmini hii inalenga kuchunguza ukamilifu na utoshelevu wa maana.

## Msingi wa nadharia

Nadharia ya Uhusiano ndiyo inatumiwa kuchanganua matini ya Pendekezo la katiba ya Kenya 2010. Nadharia ya uhusiano iliyoasisiwa na Sperber na Wilson (1986) ina misingi yake katika madai ya Grice (1975). Inadai kwamba sifa muhimu katika mawasiliano ya kibinadamu ni udhihirishaji na utambuaji wa kusudio au dhamira ya mtoa habari.

Grice alitumia kanuni mbalimbali kama vile kanuni ya ubora, ya idadi/ kiasi, ya uhusiano na kanuni ya jinsi ya kueleza makusudio. Kanuni zilizotajwa zinafaa kufuatwa na mnenaji. Grice anashikilia kuwa kutokana na kanuni ya uhusiano, kila anachokinena mnenaji lazima kiwe na uhusiano na hapa ndipo nadharia ya uhusiano ilichipuka na kuendelezwa baadaye na Gutt (1992). Sifa muhimu na ya maana inayobainisha tafsiri ni uhusiano uliopo baina ya matini lengwa na matini chasili.

Nadharia ya uhusiano ni nadharia ya kiuamuzi ya mawasiliano inayodhamiria kueleza jinsi hadhira inavyofahamu maana iliyodhamiriwa na mpasha habari. Dai la kimsingi la nadharia hii ni kuwa matamanio ya kihusiano yanayotokana na usemi au habari, yanatosha kumsaidia mpokezi kuelewa maana iliyodhamiriwa na mtoa habari. Lengo ni kueleza mchango wa matamanio ya kihusiano na vile yanavyochangia katika uelewaji unaokubalika.

Katika nadharia hii kuna mihimili inayozingatia suala la mtoa habari na jinsi anavyoweza kutoa habari yake kutosheleza kanuni zilizozungumziwa:

1. Mtoa habari anafaa kutoa habari inayosaidia kuzua athari halisi au bayana za kiutambuzi.

2. Habari inayotolewa iweze kueleweka kwa haraka bila kutumia muda mwingi kufikiria.
3. Habari inayotolewa iwe na uhusiano wa kiwango cha juu ili kufasiliwa ilivyotarajiwa.
4. Mtoa habari anafaa kuitoa habari yake kwa njia inayoeleweka kwa urahisi bila kukanganya.

Uchanganuzi wa tafsiri ya Pendekezo la katiba ya Kenya, 2010 uliongozwa na mihimili hii.

### Upekee wa sajili ya kisheria

Lugha inayotumiwa katika uandishi wa katiba ni lugha ya sheria. Hii ni lugha yenye upekee fulani na huwa tofauti na lugha ya kawaida. Kutafsiri lugha ya sheria kunahitaji makini. Ili kuelewa mambo yanayomtatiza mtafsiri katika kutafsiri lugha ya kisheria, ni vizuri kuelewa historia na asili ya lugha ya sheria inayohusika. Kama ilivyotajwa awali, katiba ya Kenya ina asili yake katika mfumo wa sheria za Waingereza ambao waliotawala Kenya kabla ya uhuru. Hakuna jawabu mwafaka la kueleza jinsi lugha ya sheria ilivyoundwa (Tiersma 1999:47). Maelezo mengi yanaweza kupatikana katika historia na matukio ambayo yameweza kuacha alama katika sheria za Kiingereza.

Lugha ya sheria huwa na msamiati wa kigeni na huhifadhi mambo na desturi za kale. Baadhi ya maneno ya kigeni yaliyo kwenye katiba ya Kenya yana asili yake katika Kiingereza. Kama ilivyo lugha ya Kiingereza, lugha ya kisheria ya Kiingereza iliathiriwa na Kijerumani wakati Waingereza na Wajerumani walipotagusana. Maneno mengi ya Kijerumani yalibaki katika lugha ya sheria ya Kiingereza. Tukio moja linalofahamika sana katika lugha ya sheria ya Uingereza lilikuwa maenezi ya ukristo mwaka wa 597 kupitia kanisa katoliki la Kirumi. Kupitia kanisa hili, lugha ya Kirumi ilipenya katika sheria za Uingereza kutokana na *canon law* iliyotumiwa katika mambo ya kanisa kama vile kutunza ndoa na familia.

Kulingana na Tiersma (1999), kuingiliwa kwa Uingereza na Wafaransa kuliathiri lugha ya sheria ya Kiingereza. Kwa mfano maneno kama vile *account, Attorney general, council* na mengine hayangetafsirika vinginevyo kwa lugha ya Kiingereza na hivyo yakaendelea kutumiwa katika lugha rasmi ya Kiingereza kama yalivyo. Kulingana na Tiersma (1999:36), maneno

yaliyoamrishwa kisheria yalikuwa muhimu sana na kuyaandika kwa lugha nyingine kulionekana kama jambo hatari na baya, kwamba yakishakubaliwa kutumiwa, maneno ya kisheria huamrisha na hayapinduliwi ovyo ovyo. Wakati mwingine maneno hayo hubaki vile vile hata kama lugha inayozungumzwa imebadilika ama hata kama watu wengi hasa umma hawaelewi maneno hayo. Mambo hayo yote hufanya lugha ya sheria kuwa nzito na yenye maneno mengi ya kikale katika Kiingereza yasiyoweza kutafsirika kwa urahisi. Mifano ya maneno iliyotolewa kama vile; *Attorney general* na *council* imetumika katika katiba ya Kenya 2010. Maneno haya yametafsiriwa katika pendekezo la katiba ya Kenya 2010 kwa kutumia njia ya maelezo. Maneno mengine ya kigeni yametafsiriwa kwa kutumia mbinu ya kukopa.

Lugha ya sheria huwa na sentensi ndefu. Sentensi ndefu husaidia kuweka habari nyingi pamoja katika usemi uliokamilika ili kupunguza utata ambao ungepatikana kama habari hiyo ingewekwa katika sentensi nyingi. Lugha ya sheria huwa na sifa ya kutumia viunganishi vingi kuunganisha vishazi. Tiersma (1999:61) anasema kuwa viunganishi hutumiwa mara nyingi sana kama vile mara tano katika lugha ya kisheria ikilinganishwa na lugha ya kawaida. Sajili ya sheria huwa na maneno mengi ambayo yana maana sawa. Jambo hili pia hutatiza mtafsiri na pia ufasili hasa kwa watu wa kawaida ambao si wanasheria.

Katika lugha ya sheria ya Kiingereza kuna matumizi ya vitenzi kama vile 'shall' ambacho kulingana na Bower (1989:35) kisheria huwa na maana ya kuamrisha au masharti. Katika Kiswahili kitenzi *shall* kinapotafsiriwa hutumiwa kumaanisha wakati ujao. Katika Kiswahili sentensi ya kawaida hutumiwa kuamrisha, jambo ambalo linaweza kupuuzwa wakati mtafsiri anatafsiri kitenzi *shall*. Newmark akinukuliwa katika Weston (1983:207), anasema maneno yanayoashiria kitu cha kipekee ama neno linaloashiria jambo ambalo ni desturi katika utamaduni wa lugha chanzi haliwezi kutafsirika. Sababu inaweza kuwa jambo hilo halipatikani katika lugha lengwa. Neno kama hilo linaweza kutafsiriwa kwa kueleza, kutumia maneno yanayokaribiana kimaana na jambo hilo, ama kwa kutumia tafsiri ya neno kwa neno pale ambapo neno hilo linaweza kubadilishwa kwa kulinyambua.

Mtafsiri hufanya tafsiri akiwa na hadhira fulani akilini mwake. Kama vile mwandishi asilia alikusudia kuathiri hadhira fulani, vivyo hivyo, mtafsiri hukusudiwa kuiathiri hadhira yake. Mtafsiri anahitaji kuwa makini katika

kuwasilisha makala kwa hadhira yake ili kuleta athari inayotarajiwa. Kwa wanasheria, kazi kuu ya mtafsiri wa lugha ya sheria ni kutoa kazi iliyo na athari sawa za kisheria katika matumizi yake. Ili kufikia lengo hilo, ni lazima anayetafsiri aweze kuelewa sio maana ya maneno na sentensi pekee bali pia athari za kisheria za maneno na sentensi hizo, na jinsi lengo hilo litaweza kufikiwa katika lugha (Sarvevic 1997). Mtafsiri wa lugha ya kisheria ni yule anayeweza kutumia lugha ya kisheria kwa njia inayofaa ili kuleta lililotakiwa na athari inayofaa. Lazima awe ni yule anafahamu vyema kanuni na mtindo wa maandishi ya kisheria katika lugha husika na utaratibu wake. Ni sharti anayetafsiri kazi ya kisheria akumbuke kwamba hata hati ya wasia huwa ni batili kama haijaandikwa kwa mtindo ufaao.

### Tafsiri ya maana asilia katika matini lengwa

Tafsiri hii ya kielelezo cha Katiba 2010 iliilenga hadhira ambayo ni watu wa viwango vyote ambao huweza kusoma na kuelewa lugha ya Kiswahili. Hawa ni watu wenye viwango mbalimbali vya elimu ambao ni pamoja na wanaoweza kusoma Kiingereza. Tofauti kati ya maana katika Matini Asilia (MA) na Matini Lengwa (ML) inaweza kuzua mtafaruku. Maana inapaswa kupewa nafasi ya kwanza katika tafsiri ya pendekezo la katiba ya Kenya 2010. Kulingana na Shitemi (1990), maana ndiyo hubebwa kutoka lugha asilia hadi lugha pokezi. Baadhi ya wataalamu kama Tytler (1790), wanadai kuwa ni jukumu la mtafsiri kupata kumwelewa zaidi mwandishi wake asilia na kujieleza katika tafsiri vile ambavyo mwandishi angejieleza angekuwa mwenyeji wa lugha pokezi. Kutokana na maelezo haya jukumu la mtafsiri ni kuhamisha maana kutoka MA hadi ML. Katika kutafsiri maana kutoka kazi asilia hadi matini tafsiri, kuna mengi yaliyojiri ikiwa ni pamoja na utata katika maana, kupotea kwa maana na maana kupotoka.

### Utata katika maana

Dhana ya utata hutokea pale ambapo kuna jambo au habari zisizoeleweka vizuri au jambo lenye maana isiyo dhahiri. Neno hili pia hutumiwa kumaanisha maana inayofahamika kuwili au kuwa na shaka kuhusu maana ya maneno. Neno au kifungu cha maneno kinaweza kuzua utata katika matumizi kulingana na muktadha.

Maana ya mwandishi huweza kupotoshwa na mtafsiri kwa kulibebesha neno moja la lugha lengwa maana nyingi mno za maneno ya lugha chasili na hivyo kusababisha utata. Kulingana na Mdee (1986), istilahi bora

hazitakiwi kubeba maana nyingi au vivuli vya maana. Kwa mfano katika maneno *application, implementation, enforcement,* na *perform* yametafsiriwa kwa kutumia neno *kutekeleza* katika MA kwenye vifungu 20, 21, 22 127 (6) (e) na 132 (3) (b).

20. ***Application*** of Bill of Right

21. ***Implementation*** of rights and fundamental freedoms

22. ***Enforcement*** of Bill of Right

127(6) (e) ***performing*** other functions

*Tafsiri:*

20. ***Utekelezaji*** wa Sheria ya Haki

21. ***Utekelezaji*** wa haki na uhuru wa kimsingi

22. ***Utekelezaji*** wa Sheria ya Haki

127 (6) (e) ***kutekeleza*** majukumu mengine

Katika mifano iliyotumika, neno moja la Kiswahili lililochaguliwa limebebeshwa maana nyingi mno kiasi kwamba wakati mwingine linapotosha maana na pia kumfanya msomaji wa ML kukanganyikiwa. Kutafsiri maneno ya Kiingereza *application, implementation, enforcement* na *perform* kuwa na maana ileile ya *kutekeleza* ni kumnyima msomaji wa ML athari inayodhamiriwa na mwandishi wa kazi asilia. Mtafsiri angetumia maelezo kutafsiri maana tofauti zinazojitokeza katika maneno ya lugha chasili. Kwa mfano neno la Kiingereza *enforcement* lina uzito zaidi ya maana kuliko neno la Kiswahili *kutekeleza.*

Matumizi ya neno kutekeleza katika kutafsiri maneno *application* na *enforcement* katika sehemu ya 20 na 22 yanaleta utata. Msomaji wa ML anaweza kufikiria kuwa mwandishi amejirudiarudia kimakosa lakini maneno haya yametumiwa kumaanisha vipengele viwili tofauti vyenye maelezo tofauti.

20. Application of Bill of Right

22. Enforcement of Bill of Right

*Tafsiri:*

20. Kutekeleza Sheria ya Haki

22. Kutekeleza Sheria ya Haki

Maneno ya Kiingereza *application* na *enforcement* yana maana tofauti. Kwa mujibu wa Longman Dictionary (1987), *application* ni neno la Kiingereza lenye

maana ya *the act of puting something into use*. Kulingana na muktadha, neno hili linaweza kuwa na maana ya 'tendo la kutumia' katika Kiswahili. *Enforcement* ni neno la Kiingereza lenye maana *to cause* ama *to make something happen, especialy by threats or force*. Katika Kiswahili neno hili linaweza kuchukuliwa kuwa na maana ya kuhakikisha kuwa jambo fulani limetendeka kwa kulazimisha. Maana ya maneno haya ni tofauti na hivyo ni makosa kutafsiriwa kuwa na maana sawa. Kuna uwezekano wa kutumia sheria bila nguvu yoyote kutumika. Kwa mfano, polisi hutumiwa kuhakikisha ya kwamba sheria zimefuatwa pale ambapo sheria zimekiukwa. Tafsiri iliyotumika katika ML inamkanganya msomaji wa ML hivyo kumfanya atafakari sana ili kuelewa tofauti ya sehemu hizo mbili. Nadharia ya uhusiano inasisitiza kuwa habari inayotolewa iweze kueleweka kwa haraka na kwa urahisi bila kukanganya. Nadharia ya uhusiano pia inasisitiza kuwepo kwa uhusiano wa hali ya juu kati ya MA na ML.

## Maana iliyopotoka

Kupotoka ni kwenda kombo au kugeuka kwa maneno, habari au maelezo. Kwa mujibu wa Bakhressa (1992), kupotoka ni kuharibika kwa maana au kitendo. Ingawa mtafsiri wa pendekezo la katiba ya Kenya 2010 amejaribu sana kuhifadhi maana ya MA katika ML, mifano iliyotolewa katika sehemu hii ni baadhi ya makosa ambayo yangeepukika. Kwa mfano katika tafsiri ya MA, uk 17 (14) (4) katika ML, uk 23 (14) (4).

> A child found in Kenya ***who is, or appears to be, less than eight years of age,*** and whose nationality and parents are not known, is presumed to be a citizen by birth.

*Tafsiri:*

> Mtoto anayepatikana nchini Kenya ambaye ***anaonekana kuwa na umri wa chini ya miaka minane,*** na ambaye uraia wake haujulikani na pia wazazi hawajulikani, atachukuliwa kuwa raia wa kuzaliwa.

Katika tafsiri hii, ujumbe katika ML unamtaja mtoto wa ***chini ya miaka minane*** haumtaji mtoto wa miaka ***minane kamili.*** Maana ni kuwa msomaji wa ML akimpata mtoto anayethibitika kuwa tayari ametimiza miaka minane, atachukulia kuwa hafai kuwa Mkenya kwa kuwa kigezo katika ML ni kutokuwa ametimiza umri huu. Hili linahitilafiana na atakayesoma MA ambayo inamtaja mtoto ambaye ametimiza miaka minane kwa kutumia maneno ***who is, or appears to be less than eight years.*** Maneno ***mtoto***

***ambaye ana umri wa miaka minane, ama ambaye anaonekana kutotimiza umri huo*** yangefaa zaidi.

Katika tafsiri ya kifungu cha MA uk. 106 (166) (2) (b) katika ML uk. 100 (166) (2) (b).

> 166. Each judge of a superior court shall be appointed from among persons who-
>
> (b) Possess the experience required under clause (3) to (6) as applicable, irrespective of whether that experience was gained in Kenya ***or in another Commonwealth*** common-law jurisdiction.

*Tafsiri:*

> 166. Majaji wa mahakama za mamlaka ya juu watateuliwa kutoka miongoni mwa watu ambao-
>
> (b) Wana tajriba inayohitajika ambayo wameipata nchini Kenya ***na taasisi nyingine za mataifa*** yanayotumia mamlaka ya sheria ya Jumuia ya Madola kama zinazotajwa katika ibara ya (3) hadi (6).

Kifungu hiki kinaleta utata kuwa MA inatoa uhuru wa mahali pa kutoa tajiriba, iwe nchini Kenya au katika mataifa mengine ya jumuia ya madola. ML inayotumia maneno ***nchini Kenya na taasisi nyingine*** inaashiria kuwa majaji wa mahakama za mamlaka ya juu wanahitajika kuwa na tajiriba kutoka Kenya na taasisi nyingine za mataifa yanayotumia mamlaka ya sheria ya Jumuia ya Madola. Matumizi ya kiunganishi 'na' katika ML inamaanisha ni lazima tajiriba inayohitajika iwe imepatikana nchini Kenya na taasisi nyingine za mataifa yanayotumia mamlaka ya sheria ya jumuia ya Madola wala si mojawapo. Jambo hili linahitilafiana na ujumbe katika MA ambayo inatoa uhuru wa chaguo la mahali pa kutoa tajiriba kwa kutumia neno ***'or'***. Maneno *Kenya **au** taasisi nyingine za mataifa yanayotumia mamlaka ya sheria ya jumuia ya Madola* yangefaa zaidi.

Mfano mwingine unahusu tafsiri ya MA uk. 112 (172) (1) (C), katika ML uk. 105 (172) (1) (c).

> Appoint, receive, complaint against, investigation and remove from office or ***otherwise discipline registrars, magistrates, other judicial officers and other staff of*** the judiciary, in the manner prescribed by an Act of ***Parliament***.

*Tafsiri:*

> Kuteua, kupokea malalamiko ya kupinga, kuchunguza na kuwafuta au ***hatua nyinginezo za kuwaadhibu, kuwasajili, mahakimu na maafisa wengine wa***

mahakama na wafanyikazi wengine wa mahakamani, ***kwa njia ambayo imetolewa na Sheria ya Bunge***

Tafsiri hii inapotosha maana asilia na kumkangaya msomaji wa ML. Neno 'wasajili' ambalo ni nomino, limebadilishwa na kuwa kitenzi-jina kwa kuongeza kinominishi awali {ku-} hivyo kubadilisha maana ya sentensi nzima na kusababisha utata. Pia, matumizi ya kipumuo baada ya neno 'kuwaadhibu' ni makosa kwa sababu maana inabadilika. Kulingana na muktadha, neno 'wasajili' linaeleweka kama watu ambao wanatarajiwa kufanya kitendo cha kusajili. Kitendo cha kusajili hakiwezi kuadhibiwa bali wanaofanya kitendo hicho cha 'kusajili' ndio wanaweza kuadhibiwa pamoja na maafisa wengine waliotajwa. Maneno ***'or otherwise discipline registrars'*** yaliyoeleweka na mtafsiri kama, ***au hatua nyinginezo za kuwaadhibu, kuwasajili*** yalifaa kutafsiriwa kama; au vinginevyo kuwaadhibu wasajili, ili kifungu kiwe; Kuteua, kupokea malalamiko ya kupinga, kuchunguza na kuwafuta ***au vinginevyo kuwaadhibu wasajili, mahakimu na maafisa wengine wa mahakama na wafanyikazi wengine wa mahakamani, kwa njia ambayo imetolewa na sheria ya bunge.***

Maana asilia ya mwandishi pia imepotoka katika tafsiri ya MA uk. 67 (100) (e), maneno ambayo yametafsiriwa kama ifuatavyo katika ML uk. 65 (100) (e).

(100). Parliament shall enact legislation to promote the representation in parliament of-

(e) Marginalised communit*ies.*

*Tafsiri:*

(100). Bunge litatunga sheria kuimarisha uwakilishwaji Bungeni wa-

(e) jamii iliyotengwa.

Katika kifungu hiki, kutafsiri maneno ***marginalised communities*** kama ***jamii iliyotengwa*** ni kupotosha kwa sababu dhana ya jamii moja pekee inaibuka katika tafsiri. Msomaji wa ML hatarajii jamii nyingi zitafutiwe uwakilishwaji kama inavyodhamiriwa na kifungu hicho. Msomaji huyu anatarajia jamii moja pekee iliyotengwa itafutiwe uwakilishwaji. Kwa msomaji wa ML kutafutiwa uwakilishwaji kwa jamii nyingi kutaleta mtafaruku. Neno la Kiingereza *communities* lenye maana ya jamii nyingi limeundwa kutokana na neno la Kiingereza *community* lenye maana ya jamii moja. Mofu '-ies' ni mnyambuliko wa Kiingereza unaoleta dhana ya wingi. Dhana ya wingi katika

Kiswahili huonyeshwa kwa kutumia viambishi ngeli katika upatanisho wa kisarufi. Maneno ***jamii zilizotengwa*** yangefaa zaidi.

## Maana iliyopotea

Kwa mujibu wa TUKI (1981), kupotea ni kukosekana kwa kitu au jambo ama kosa kufuata njia inayofaa. Ni jukumu la mtafsiri kuhakikisha kwamba anahifadhi maana ya mwandishi asilia. Kwa mujibu wa Mwansoko (1996), uaminifu wa mtafsiri wakati mwingine hupotea kwa kupunguza vipengee au hata maneno kadhaa katika kazi yake katika jitihada za kujaribu kufafanua au kueleza maana ya baadhi ya maneno ya mwandishi. Tafsiri haiwezi kuwa kamili au sahihi ikiwa sehemu fulani ya maana asilia inakosekana katika matini lengwa. Kwa kuzingatia tafsiri ya MA uk. 29 (36) (1) katika ML uk. 33 (36) (1), ujumbe haujawasilishwa kikamilifu.

> 36 (1) Every person has the right to freedom of association, which includes the right to form, join or participate in the activities of an association *of any kind.*

*Tasfsiri:*

> 36 (1) Kila mtu ana haki ya uhuru wa kutangamana ambayo inahusu haki ya kuanzisha, kujiunga na, au kushiriki katika ***majukumu ya mashirika***.

Maneno ***association of any kind*** yametafsiriwa kama ***mashirika*** katika ML maneno *of any kind* hayajajitokeza katika maana, hivyo msomaji wa ML hapati dhana ya ***mashirika ya aina yoyote***, ambayo ilidhamiriwa na MA. Maana yake, anayesoma ML atadhani kuwa kunayo mashirika fulani anayokubaliwa kujiunga nayo, kinyume na ilivyo katika MA.

Mfano mwingine ni tafsiri ya MA uk 33 (45) (2) katika ML uk 37 (45) (2).

> Every adult has the right to marry a person of the opposite sex, based on the ***free consent*** of the parties,

*Tafsiri:*

> Kila mtu mzima ana haki ya kuoa mtu wa jinsia tofauti na yake na kulingana na ***makubaliano*** yao.

Katika kifungu hiki neno *free* lilipuuzwa na mtafsiri kwani maana ya neno hili haijitokezi katika ML. Jambo hili linamyima msomaji wa ML ujumbe kamili. Maana ***makubaliano ya hiari/huru*** inayotokea katika MA haitokei

katika ML. Kuna hatari kwa msomaji wa ML kuelewa kuwa makubaliano yoyote, yawapo ya kusukumiwa yanampa mtu haki ya kuoa au kuolewa na mtu mzima mwingine. Hii ni kwa sababu mtafsiri alipuuza uzito wa neno la Kiingereza *free* lililotumiwa na mwandishi wa matini chasili.

## Baadhi ya vifungu au maneno yasiyotafsiriwa

Ni jambo la muhimu kwa mtafsiri kuhakikisha kuwa maana asilia ya matini chasili imejitokeza katika kazi yake, la sivyo, tafsiri yake itakuwa na upungufu. Tafsiri haiwezi kuwa sahihi wala kamili ikiwa sehemu fulani ya maana asilia inakosekana katika matini lengwa.

Mfano mwingine ni katika tafsiri ya MA uk. 81 (131) (2) (d), na ML uk. 78 (131) (2) (d).

The president shall-
promote respect for the diversity of the people and ***communities*** of Kenya.

*Tafsiri:*

Rais-
atakuza heshima ya uanuwai wa watu wa Kenya.

Maneno ***and communities*** yaliyo na maana ya ***na jamii*** hayakutafsiriwa katika kifungu kilichoonyeshwa. Inaonekana kuwa mtafsiri alichukulia kuwa maneno ***people*** na ***communities*** yana maana sawa ilhali sivyo. Neno jamii ni mahususi kuliko watu ambalo ni la jumla, hivyo lilifaa kutafsiriwa ili uanuwai uliodhamiriwa na MA ulenge maana ya jamii za Kenya ila sio 'watu' tu.

Maneno katika sehemu 230 (1) iliyo katika MA hayakutafsiriwa katika ML 230 (1).

230 (1). There is established the Salaries and Remuneration Commission.

Sentensi hii nzima haijatafsiriwa na hivyo ujumbe huu ambao unapatikana katika MA kukosekana katika ML.

Kifungu cha MA, uk. 116 (180) (6), hakikutafsiriwa katika ML.

(180) (6) The Independent Electoral and Boundaries Commission shall not conduct a separate election for the deputy goverment but shall declare the candidate nominated by the person who is elected county governor to have been elected as the deputy governor.

Kifungu hiki kizima hakijatafsiriwa katika ML uk. 108 (180). Haya ni makosa kwa sababu mtafsiri hakuhifadhi ujumbe wa mwandishi asilia. Ujumbe wa kifungu hiki haupatikani katika ML kwa sababu mtafsiri hakukishughulikia kabisa.

### Msamiati na tahajia

Kulingana na makala haya, msamiati ni jumla ya maneno yanayotumiwa katika lugha. Neno ni kipashio kimojawapo kati ya vile vinavyojenga lugha (Oser 1989). Ni muhimu mtafsiri ahakikishe kuwa amewasilisha maana vizuri ili iweze kueleweka mara moja, na kwa njia inayoweza kuleta athari sawa na maana chasili kama ilivyokusudiwa na mwandishi asilia. Ili kuhakikisha hili, kipengele cha msamiati kinafaa kuzingatiwa. Katika sehemu hii kipengele cha msamiati kimechunguzwa katika kiwango cha maana katika ML ili kuona ilivyowasilishwa kutoka kwa MA. Mfano wa kwanza tunaozingatia unapatikana katika MA uk.18 (15) (1) na ML uk. 23 (15) (1).

> A person who has been ***married*** to a citizen for a period of at least seven years is entittled on application to be registered as a citizen.

*Tafsiri:*

> Mtu ambaye ***ameolewa*** na raia kwa muda wa angalau miaka saba ana haki ya kutuma maombi ya kusajiliwa kama raia.

Katika sentensi hii, neno la Kiingereza *married* lililotumiwa katika MA lina maana ya ***kuoa na kuolewa.*** Katika ML neno hili limetafsiriwa kumaanisha kuolewa. Ujumbe katika MA unarejelea wote wawili, yaani mke aliyeolewa na raia Mkenya kwa miaka saba na mume ambaye ameoa raia wa Kenya kwa miaka saba. Maana ambayo inajitokeza katika ML ni kuwa mwanamume aliyemuoa mke Mkenya hawezi kusajiliwa kuwa Mkenya na sivyo ilivyo katika MA. Maana imepungukiwa kwa sababu mtafsiri hakutilia maanani maana kamilifu ya neno *married* katika lugha ya Kiswahili.

Mfano mwingine unapatikana katika tafsiri ya MA uk. 25. (26) (2) katika ML uk. 30 (26) ( 2).

> The life of a person begins ***at*** conception.

*Tafsiri:*

> Maisha ya mtu huanza ***baada ya*** kutunga mimba.

Kutafsiri maneno ***at conception*** kuwa na maana ya ***baada ya kutunga mimba*** kunapotosha maana. Kipashio *at* kina maana tofauti na *baada ya*. Kipashio *at* katika MA kinamaanisha ya kwamba uhai huanza wakati mimba inapotungwa. Ujumbe katika ML unazua dhana kuwa wakati mtoto anatungwa uhai haupo ila baada ya kukamilika kutungwa kwa mimba. Tafsiri ingekuwa *mimba inapotungwa* au *wakati mimba inatungwa*.

## Tahajia

Mtafsiri anafaa kuihariri kazi yake kikamilifu ili kuepuka makosa ya hijai ambayo yakiwapo yanaathiri au kupotosha maana kusudiwa. Tahajia ni uwakilishaji wa sauti kwa herufi katika maandishi kufuatana na muendelezo wa maneno uliokubaliwa (TUKI 1981). Mtafsiri wa pendekezo la Katiba ya Kenya 2010 amejitahidi vilivyo kuepukana na makosa ya tahajia. Hata hivyo kuna makosa machache yanayojitokeza na kuleta mkanganyo katika maana. Kwa mfano neno *kutangaza* katika ML kifungu (132) ( e) limechapwa kama *kurangaza*.

> 132. 4. The President may –
>
> (e) with approval of parliament, declare war.

*Tafsiri:*

> 132.( 4) Rais anaweza-
>
> (e) kwa idhini ya Bunge, anaweza ***kurangaza*** vita.

Msomaji wa ML ambaye hajafahamu vizuri maneno ya Kiswahili anaweza kufikiria kuwa neno hilo *kurangaza* ni msamiati wa Kiswahili. Neno *mahakama* katika ML 140 (2) limeandikwa kama ***mahakaya*** ya juu.

> 140. (2). Within fourteen days after the filing of a petition under clause (1), the supreme court shall hear and determine the petition and its decision shall be final.

*Tafsiri:*

> 140. (2). Katika muda wa siku kumi na nne baada ya kuwasilishwa kwa malalamiko, ***Mahakaya*** ya juu itasikiza na kuamua kesi hiyo na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

Mfano mwingine ni neno *mwanachama* katika ML kifungu 88 (2) limechapwa kama ***mwachama***.

88. (2). A person is not eligible for apointment as a member of the Commission if the person...

*Tafsiri:*

88. (2). Mtu hastahili kuteuliwa kama ***mwachama*** wa Tume, ikiwa mtu huyo...

Kazi ya kisheria hutajwa kwa kurejelea nambari ya kifungu, ibara fulani au sehemu fulani. Makosa katika kuandika nambari kunaweza kuwatatiza wasomaji hasa wakati wa kurejelea. Mfano wa makosa kama haya ni katika tafsiri ML 75 (2) (a) na (b), ikilinganishwa na MA 75 (2) (a) na (b).

75. (2) A person who contravenes Clause (1), or Article 76, 77, or 78 (2)-

(a) shall be subject to applicable disciplinary procedure for the relevant office; and

(b) may, in accordance with the disciplinary procedure referred to in pharagraph (a), be dismissed or otherwise removed from office.

*Tafsiri:*

75. (2) Afisa wa Serikali anayetenda kinyume na ibara ya (1) au kifungu cha 76, 77, au 78 (2)-

(d) atawekwa chini ya taratibu za kinidhamu zinazotumika kwa afisi inayotumika;

(e) kulingana na taratibu za kinidhamu zilizotajwa katika aya (a), anaweza kuachishwa kazi au vinginevyo, kuondolewa afisini.

Katika tafsiri hii, **(d)** na **(e)** zimetumiwa badala ya **(*a*)** na **(*b*)**. Makosa kama hayo pia yamefanywa katika tafsiri ya kifungu 83 (1) (a), (b) na (c) ikilinganishwa na MA 83 (1) (a), (b) na (c). Pia katika kifungu 172 (1) kuna sehemu (c) mbili zenye maelezo tofauti. Msomaji wa ML anaporejelea sehemu hizi atakuwa anaongea kuhusu mambo tofauti na ujumbe ulio katika sehemu hizo kwenye MA. Makosa haya yanapatikana katika sehemu kadhaa za ML. Kwa mfano sehemu 230 (2) katika MA, imeandikwa katika nafasi ya 230 (1), ambayo haikutafsiriwa katika ML.

Mtafsiri ametunza muundo wa MA kwa kiwango kikubwa katika tafsiri yake. Kazi iliyotafsiriwa inaeleweka kuwa ya kisheria, inasomeka kwa urahisi na kueleweka kwa urahisi isipokuwa baadhi ya sehemu zilizotajwa kuwa na mushkili katika kazi hii. Kueleweka kwake pia ni kwa sababu matini zote mbili zimeandikwa na kutumika katika mazingira sawa ambamo lugha zote mbili zinatumika. Ukubwa wa tafsiri karibu unalingana na ukubwa

wa kazi ya MA. Mtafsiri amejaribu awezavyo kutumia maneno ya kawaida au yaliyozoeleka ili kurahisisha kuhisika kwa maana.

## Hitimisho

Lengo la makala haya lilikuwa kutathmini ukamilifu wa maana katika matini lengwa. Makala haya yamebainisha kuwa lugha ya sheria ni yenye urasmi mwingi na haibadiliki, ina msamiati wa kipekee, huwa na sentensi ndefu, na viunganishi vingi. Kwa sababu hii, tafsiri ya sajili ya sheria inahitajika kufanywa kwa uangalifu.

Makala yamebainisha kwamba tafsiri ya kielelezo cha Katiba 2010 ilikuwa na matatizo yaliyosababisha upotoshi wa maana. Kwa mfano, utata umetokea pale ambapo mtafsiri ametumia neno au kifungu cha maneno kueleza maana tofauti na maana iliyo katika MA. Baadhi ya maneno na vishazi yametafsiriwa kwa jinsi ambayo inayomkanganya msomaji wa ML ikilinganishwa na maana katika MA. Kazi hii inadhihirisha kwamba kuna mabadiliko ambayo yamefanywa na mtafsiri na kusababisha kupotoka kwa maana. Maneno kadhaa yasiyofaa yametumiwa kama visawe vya baadhi ya vifungu na maneno na hivyo kupotosha maana katika ML.

Kuna mabadiliko ambayo yametokea na kusabasisha kupotea kwa maana. Mtafsiri ametumia maneno ambayo hayawasilishi maana kamili ya MA. Maana pia imepotea kupitia maneno na vifungu ambavyo havikutafsiriwa kabisa katika ML. Katika kila kiwango kilichoshughulikiwa, maana ya MA imeathirika kwa kiwango fulani.

Katika kiwango cha msamiati imebainika kuwa kuna baadhi ya maneno ambayo yametafsiriwa kwa jinsi inayopotosha na kupoteza maana. Baadhi ya maneno yameendelezwa kwa njia isiyofaa na kusababisha utata. Mabadiliko yaliyotokea katika MA na ML yanaweza kuwa yametokana na tofauti za lugha mbili husika. Tofauti pia zanaweza kuwa zimetokana na nia ya mtafsiri kutaka kueleza yaliyomo katika MA kwa njia ambayo inakubalika na hadhira pokezi ama uwezo wa mtafsiri.

Kwa jumla kuna mabadiliko yaliyotokea katika baadhi ya sehemu za tafsiri na kuathiri maana ya MA kwa kiwango fulani. Hata hivyo, athari hizi zilizotokea kwenye baadhi ya maana za MA hazifanyi matini tafsiri kuonekana kama isiyotokana na MA. Hii ni kwa sababu matatizo hayo hayazuii mawasiliano kwa kiwango kikubwa. Isipokuwa sehemu chache ambazo zimetajwa kuwa na matatizo, inabainika kuwa watafsiri wa

pendekezo la katiba ya Kenya 2010 walijitahidi kuwasilisha ujumbe wa kazi asilia.

Kazi yoyote ya kubadili matini ya lugha chasili kuwa sawa na ya lugha lengwa ni kazi ngumu. Mtafsiri wa pendekezo la katiba ya Kenya 2010 alijaribu kuwasilisha ujumbe awezavyo. Kando na upungufu uliopatikana, utafiti huu unasisitiza kuwa tafsiri ya katiba ni muhimu na ni kitu cha thamani kubwa kwa Wakenya. Hivyo basi kuna umuhimu wa kutafsiri kwa makini.

## Marejeleo


Bakhressa, S. K. (1992). *Kamusi ya Maana na Matumizi*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Bower, F. (1989). *Linguistic Aspect of Legislative Expressions*. Vancouver: University of Columbia Press.

Grice, H.P. (1989). *Studies in the Way of Words*. Cambridge: Harvard University Press.

Gutt, E.A. (1992). *Relevance Theory: A Guide to Successful Communication in Translation*. Dallas: Summer Institute of Linguistics.

Gicheru, H.B. and Miano, K. (1987). *A Textbook of the Constitution and Government of Kenya for Secondary Schools*. Nairobi: Sterling Publishers.

Kibwana, K, Peter C.M. na Bazaara, N. (2001). *Constitutionalism in E.A.* Kampala: Fountain Publishers Ltd.

Kibwana, K. (1997). *Introduction to the Constitution of Kenya*. Nairobi: Claripress Ltd.

Kindiki, K. and Ambani, O. (2005). *The Anatomy of Bomas: The Selected Analysis of 2004 Draft Constitution of Kenya*. Nairobi: Claripress Ltd.

Mdee, J.S. (1997). *Nadharia na Historia ya Lesikografia*. Dar es Salaam: TUKI.

Melvin, E. (2010). c:/Documents and Setings /Eric Melvin Document/ Constitution.

Mwansoko, H. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadhria na Mbinu*. Dar-es-Salaam: TUKI.

Newmark, P. (1981). *Approaches to Translation*. Oxford: Pergamon Press.

Oser, E. (1987). 'International Organizations' in *The Translators Handbook*. Catriona Pickon (2nd Edition). Aslib Publisher New York Press.

Sperber, D na Wilson, D. (1986). *Relevance: Communication and Cognition*. Oxford: Blackwell.

______(1995). *Post face to the second edition of Relevance*. Communication and Cognition. Oxford: Blackwell.

Sarcevic, S. (1997). *A New Approach to Legal Translation*. The Hague: Kluwer l Law International.

Shitemi, N.L. (1990). "Mawasiliano katika Tafsiri. Utenzi wa mtafsiri". Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Tiersma, P. (m.) (1989). Aspect of Legislative Expression. Vancouver: University of British Columbia.

TUKI (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Tytler, A.F. and Woodhousel, L.(1790). *Essays on the Principles of Translation*. Amsterdam: John Benjamin B.V.

Wilson, D. na Sperber, D. (2004). 'Relevance Theory' in Ward'. In G. and Horn, L (Eds) *Handbook of Pragmatics*. Oxford: Blackwell, 607-632.

Weston, M. (1983). 'Problems and Principles in legal Translation', The Incoporated Linguistic. *Autumn* vol 22, No 4.